**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents MoFP Budget

2021-06

# Hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Makadirio ya Mapato na matumizi 2021 - 2022

Tanzania, Jamhuri ya Muungano

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/228

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

## HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB.), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2021/22

**DODOMA** **JUNI 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/21 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya, na pia kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine kujadili bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/22. Kipekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mbunge wa Muhambwe (CCM) na Mheshimiwa Kavejura Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe (CCM) kwa kuchaguliwa kwao kuwa wawakilishi wa wananchi wa majimbo yao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana kwa kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Muhambwe na Buhigwe.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukushukuru wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuendesha vema majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2021/22. Aidha, ninaipongeza kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Sillo Daniel Baran – Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Omari Mohamed Kigua – Mbunge wa Kilindi kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/22.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu itajikita katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni: majukumu ya Wizara; mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/21; vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2021/22; na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2021/22.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili 2016, majukumu ya kisera na kiutendaji ya Wizara ya Fedha na Mipango yanatekelezwa kupitia Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi, Fungu 21 – HAZINA, Fungu 22 - Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Majukumu hayo ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla;

(ii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu, mifumo na miongozo ya Fedha;

(iii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira, Mipango, Mikakati na Miongozo ya Maendeleo ya Taifa;

(iv) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

(v) Kudhibiti na kusimamia ulipaji wa Deni la Taifa;

(vi) Kudhibiti na kusimamia mali na vyombo vya Serikali ;

(vii) Kusimamia uendeshaji wa Mashirika ya Umma pamoja na vitega uchumi vya Serikali;

(viii) Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wasio wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(ix) Kusimamia masuala ya ukaguzi wa mapato, matumizi na mali za Serikali;

(x) Kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi; na

(xi) Kukusanya, kuchakata, kuandaa, kusambaza na kusimamia matumizi ya takwimu rasmi za Taifa.

# 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/21

## 3.1 Mapitio ya Mapato na Matumizi

### 3.1.1Mapato

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 973.02 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo gawio, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, marejesho ya mikopo, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 533.18 sawa na asilimia 54.7. **Jedwali Na.1**

**Jedwali Na.1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kati ya Julai 2020 na Aprili 2021**

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti 2020/21 | Kiasi kilichokusanywa hadi Aprili | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 931,065,159,090 | 478,177,000,000 | 51 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 41,791,905,888 | 54,886,201,391 | 131 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 158,000,000 | 117,934,000 | 75 |
| **JUMLA** | | **973,015,064,978** | **533,181,135,391** | **55** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

### 3.1.2 Matumizi

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 12.48 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.81 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 670.00 ni matumizi ya maendeleo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yametumia jumla ya shilingi trilioni 8.42 sawa na asilimia 67.48 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotumika, shilingi trilioni 8.38 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 37.36 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika **kiambatisho Na. 1– 3.**

## 3.2 Utekelezaji wa Majukumu

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2020/21 unaendelea kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

i. Kuimarisha usimamizi wa sera za uchumi jumla ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa na kudhibiti mwenendo wa mfumuko wa bei ili ubaki katika wigo wa tarakimu moja;
ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mikakati, mpango na bajeti ya Serikali;
iii. Kuunganisha na kuhuisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo na kuimarisha usimamizi wa fedha na mali za umma;
iv. Kushirikiana na Wizara za kisekta, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretatieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao;
v. Kuwajengea watumishi uwezo wa kutumia mifumo ya fedha iliyoundwa na kuhuishwa, ili kuongeza tija katika usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali;
vi. Kuanzisha kituo cha ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *PPP Center;*
vii. Kuratibu majadiliano ya misaada na mikopo kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, benki na taasisi za fedha za kimataifa;
viii. Kukamilisha na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030), Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha; na
ix. Kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu mbalimbali za kuwajengea wananchi uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini, hususan umaskini wa kipato.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Julai 2020 na Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo;

### 3.2.1 Kuandaa na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2020/21, Wizara imeendelea kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kufanya yafuatayo: Kutoa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo; kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi, hususan miradi ya kielelezo na kimkakati; kuchambua na kutoa hati 834 za msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kulipa malimbikizo ya madai na madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi, watumishi, wazabuni na watoa huduma pamoja na marejesho ya Kodi ili kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi; na kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki za biashara pindi zinapokopa kutoka Benki Kuu (discount rate) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 5 pamoja na kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania (Statutory Minimum Reserve Requirement) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6 kwa lengo la kuongeza ukwasi katika sekta ya benki.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Benki Kuu imeendelea kutumia nyenzo mbalimbali, ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la jumla la fedha za kigeni ili kudhibiti mfumuko wa bei pamoja na hali ya ukwasi katika soko. Aidha, pamoja na athari za Ugonjwa unaosababishwa na Virus vya Korona – 19, udhibiti thabiti wa ukwasi katika soko umewezesha ukuaji chanya wa mikopo kwa sekta binafsi kwa wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka unaoishia Aprili 2021, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imetokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, hususan utalii, usafirishaji na

huduma za chakula na malazi.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na usimamizi madhubuti wa sera za uchumi jumla, ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa na matokeo chanya ya wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka 2020, ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji umetokana na athari za UVIKO - 19 katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, katika mwaka 2020, sekta zilizokua kwa viwango vya juu ni pamoja na: Sekta ya Ujenzi (asilimia 9.1); Habari na Mawasiliano (asilimia 8.4); Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 8.4); Huduma zinazohusiana na Utawala (asilimia 7.8); Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi (asilimia 7.3); Madini na Mawe (asilimia 6.7); na Afya na Huduma za Jamii (asilimia 6.5).

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa viashiria vingine hadi mwezi Aprili ni kama ifuatavyo: Mfumuko wa bei uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja (1) wa wastani wa asilimia 3.3, ikiwa ni chini ya lengo la asilimia tano (5); kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kwa nchi, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); na nakisi ya bajeti inatarajiwa kutozidi asilimia 2.6 kutokana na mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali.

### 3.2.2 Kuandaa na Kusimamia Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali

#### 3.2.2.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 -2025/26).

Mpango huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na mipango na mikakati ya kikanda na kimataifa.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kukamilisha kazi zifuatazo: (i) Maandalizi ya Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21; (ii) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambao uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu Aprili 2021; (iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ambao ulijadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Machi 2021, na unatarajiwa kuwasilishwa hivi karibuni Bungeni; Maandalizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo *(National Projects Management information System – NPMIS)* pamoja na mafunzo ya mfumo huo kwa watumishi 219 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi 95 ya maendeleo, ikijumuisha miradi 58 ya kimkakati, miradi tisa (9) inayotekelezwa na Sekta Binafsi na miradi 28 ya kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za miradi tisa (9) ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali; maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo; na Mapitio ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu.

### 3.2.2.2 Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

#### 3.2.2.2.1 Mapato

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia hatua mbalimbali za kodi zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kazi

zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha Mkakati wa Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani 2020/21 – 2024/25; kuchambua na kutoa hati 787 za msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa miradi ya maendeleo 587; kusimamia uchambuzi na marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; pamoja na mapitio ya mikataba 983 ya ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kuhusu masuala ya kodi.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi madhubuti wa hatua za kodi na mikakati ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi umeiwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi trilioni 16.95, sawa na asilimia 86.0 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 19.72 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 14.54, sawa na asilimia 86.9 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 16.74, mapato yasiyo ya kodi kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yamefikia shilingi trilioni 1.80, sawa na asilimia 78.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.30; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 607.41, ikiwa ni asilimia 88.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 686.22 katika kipindi hicho.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kusimamia na kuratibu upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 4,949.25 kutoka katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,992.71, sawa na asilimia 95.7 ya lengo la kokopa shilingi bilioni 4,170.01 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,675.63 zimegharamia mikopo ya ndani iliyoiva na shilingi bilioni 1,317.08 zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 3,035.6 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi ya maendeleo. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mkopo wa jumla ya shilingi bilioni 1,683 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia katika bajeti ya Serikali shilingi bilioni 2,874.37. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 949.32 ni misaada na shilingi bilioni 1,925.04 ni mikopo nafuu. Hadi Aprili 2021, Washirika wa Maendeleo wametoa jumla ya shilingi bilioni 1,894.96, sawa na asilimi 70 ya makadirio ya kipindi hicho ya kuchangia shilingi bilioni 2,692.0. Kati ya kiasi hicho, misaada ya kibajeti ni shilingi bilion 210.24, sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho, miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,454.72, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,287.98 na mifuko ya kisekta shilingi bilioni 230.0, sawa na asilimia 87 ya makadirio ya shilingi bilioni 265.69 ya kipindi hicho.

#### 3.2.2.2.2 Matumizi

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, Wizara imeendelea kuzingatia taratibu za kutoa, kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Hadi Aprili 2021, jumla ya shilingi trilioni 24.74 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 7.32 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 6.84 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali, shilingi trilioni 6.09 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**22.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kufanya uhakiki na kulipa madai mbalimbali ya watumishi, wakandarasi, washauri elekezi pamoja na fidia kwa miradi ya

barabara, madaraja, viwanja vya ndege na miradi ya maji. Hadi Aprili 2021, madai yenye jumla ya shilingi bilioni 965.1 yamehakikiwa na kulipwa. Kati ya kiasi hicho, madai ya wakandarasi ni shilingi bilioni 704.5, wazabuni shilingi bilioni 21.6, watumishi shilingi bilioni 97, madeni mengineyo shilingi bilioni 92.1, watoa huduma shilingi bilioni 34.2 na fidia kwa wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ni shilingi billioni 15.7.

### 3.2.3 Usimamizi wa Deni la Serikali

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia deni la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134. Hadi Aprili 2021, Wizara imelipa deni lote lililoiva lenye thamani ya shilingi trilioni 6.84. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.10, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.42 na mtaji shilingi trilioni 2.68. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni 2.74, ikijumuisha riba ya shilingi trilioni 0.63 na mtaji shilingi trilioni 2.11.

**24.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kazi nyingine zilizofanyika ili kudhibiti deni la Serikali ni pamoja na: Kuhuisha Mkakati wa Muda wa Kati wa Usimamizi wa Deni wenye lengo la kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali; kukamilisha Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi na Utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada wa mwaka 2020; na kufanya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni Novemba 2020, ambayo imeonesha kuwa, viashiria vya deni la Serikali vipo ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

### 3.2.4 Usimamizi wa Mafao ya Wastaafu na Mirathi

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia mafao na pensheni kwa watumishi wa Serikali ambao siyo wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii, pamoja na mirathi

na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa. Hadi Aprili 2021, Wizara imewezesha malipo ya mafao na pensheni kwa wastani wa wastaafu 57,351 kila mwezi, mirathi kwa warithi 1,187, malipo ya malezi kwa walezi 1,035 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba 482. Aidha, Wizara inaendelea kufanya uhakiki wa wastaafu wote Tanzania nzima wanaopata malipo ya pensheni kupitia Hazina.

### 3.2.5 Kusimamia Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na Mali za Umma;

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2021, Wizara imefanya yafuatayo: Kuandaa Mpango wa Wizara wa Kuwezesha Upatikanaji wa Huduma za Mifumo ya Kifedha wakati wa Majanga; kuunganisha watoa huduma 135 kwenye mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG) ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuandaa Mkakati wa Serikali wa Kusimamia Mifumo ya Taarifa za Fedha; kuboresha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato - GePG ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za malipo; na kuunganisha Mfumo wa Ulipaji Serikalini – MUSE. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia mifumo mingine ya kieletroniki ya kifedha ambayo ni Mfumo wa Taarifa za Mishahara Serikalini - GSPP, Mfumo wa Kupanga Rasilimali Serikalini - GERAS, Mfumo wa Mipango na Taarifa - PLANREP, Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti ya Serikali - CBMS, Mifumo ya kielektroniki ya Benki Kuu ya Tanzania na Benki za Biashara, hususan NMB na CRDB.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na: kufanya maboresho ya Moduli mbili (2) za uondoshaji wa mali chakavu na usimamizi wa ajali na fidia; kuingiza kwenye mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali

(GAMIS) mali zenye thamani ya shilingi trilioni 25.42 katika taasisi 394; kufanya uhakiki wa mali kwenye vituo 117 katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali; na kufanya uhakiki maalumu wa vyombo vya kuhifadhia fedha, mali za thamani na nyaraka muhimu za Serikali, ambapo uhakiki umefanyika kwa vyombo na vifaa 137. Aidha, taasisi 551 zimeunganishwa kwenye mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

### 3.2.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

**28.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kukamilisha taratibu za kuanzisha Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Hadi Aprili 2021, Wizara imekamilisha taratibu zote za uanzishwaji wa kituo. Kazi nyingine zilizofanyika ni kuchambua na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Mradi wa Kuunganisha Simu za Viganjani unaoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), Mradi wa Hoteli ya Nyota Nne na Mradi wa Jengo la Biashara inayotarajiwa kujengwa kwenye Uwanja wa Ndege wa JNIA. Miradi hii ipo katika hatua za ununuzi wa wabia.

### 3.2.7 Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kampuni tanzu zilizoanzishwa na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanaonesha kuwa, jumla ya taasisi na mashirika ya umma 23 yamefanya uwekezaji kwa kuanzisha kampuni tanzu 57; taasisi na mashirika 22 yamefanya uwekezaji wa ubia na nyingine kununua hisa kwenye kampuni binafsi 79. Ili kuimarisha usimamizi wa kampuni tanzu, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaandaa mwongozo utakaobainisha mambo muhimu ya kuzingatia katika kuanzisha, kuendesha na kusimamia

kampuni tanzu zitakazoanzishwa na taasisi na mashirika ya umma.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina imehaulisha na kuboresha mfumo wa Mipango na Utoaji wa tarifa - PLANREP unaotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumika katika uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa taasisi na mashirika ya umma. Aidha, hadi Aprili 2021, jumla ya taasisi na mashirika 229, kati ya 237 yameanza kutumia mfumo huo katika kuandaa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2021/22. Kazi nyingine iliyofanyika ni majumuisho ya mabadiliko ya Sheria ya Msajili wa Hazina, SURA 370 kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 3.2.8 Usimamizi wa Sekta ya Fedha

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi na mamlaka za usimamizi na udhibiti katika kusimamia na kuendeleza sekta ya fecha. Shughuli zilizotekelezwa hadi Aprili 2021 ni pamoja na kusimamia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka 10; masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa; huduma za bima; Taasisi za Benki; uwekezaji wa pamoja; na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

#### 3.2.8.1 Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030)

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kuzindua na kusambaza Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030) pamoja na Mpango Kazi wa utekelezaji; kuandaa Mpango wa Elimu ya Fedha wa Mwaka 2021-2025 na nyenzo za kufundishia; kuendelea kusimamia Sera, Sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha ambapo Benki

Kuu ya Tanzania imetoa leseni kwa Kampuni 415 za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 230 na Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za kifedha 2,254; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha hususan, kwa wahariri wa vyombo vya habari, wabunge, watendaji wa mikoa, waratibu 212 wa huduma ndogo za fedha kwa ngazi ya wizara, mkoa, wilaya, wahadhiri wa vyuo vya elimu ya juu pamoja na wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha.

### 3.2.8.2 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**33.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA ina jukumu la kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: kuchambua na kuidhinisha maombi ya kuorodheshwa kwa hisa 2,164,349 za Kampuni ya JATU zenye thamani ya shilingi bilioni 1.08; maombi ya kuuza hisa 24,509,804 za Benki ya Mufindi zenye thamani ya shilingi bilioni 5; na kuuza hisa 174,500,000 za Benki ya Biashara ya NMB zenye thamani ya shilingi bilioni 420.5 kutoka Kampuni ya Rabobank kwenda Kampuni ya Arise. Aidha, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma za masoko ya mitaji kwa wananchi mijini, vijijini na nje ya nchi, Mamlaka imechambua na kuidhinisha matumizi ya Mfumo wa Kuuza na Kununua Hisa kwa njia ya simu za mkononi (DSE Mobile Trading Platform - Hisa Kiganjani)

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni kutoa leseni 144 kwa watendaji na washauri wa uwekezaji katika masoko ya mitaji. Kati ya leseni 144, leseni zilizotolewa kwa ajili ya Soko la Hisa ni moja (1), Soko la Bidhaa moja (1), Hifadhi Kuu ya Dhamana moja (1), Madalali wa Soko la Hisa

12, Watendaji katika Soko la Bidhaa tano (5), Watendaji katika Soko la Hatifungani sita (6), Washauri Wateule sita (6), Washauri wa Uwekezaji 14, Mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja tisa (9), Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja 10, Watunza Dhamana sita (6), na Wawakilishi wa Taasisi zinazotoa huduma katika Masoko ya Mitaji 73.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Soko la Bidhaa Tanzania - TMX imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau juu ya faida na umuhimu wa kutumia mtandao wa Soko la Bidhaa katika kuuza na kununua mazao. Hadi Aprili 2021, Soko la Bidhaa limewezesha uuzaji na ununuzi wa mazao ya choroko, Dengu, Korosho na Ufuta kwa njia ya mtandao. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na: kuongeza moduli ya mshindi wa zabuni na upatikanaji wa taarifa za minada iliyopita kwenye mfumo wa Soko la Bidhaa kwa urahisi wa rejea; na kutoa elimu kwa wadau 780, wakiwemo viongozi wa AMCOS, Maafisa Kilimo viongozi wa Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Maafisa Ushirika na Warajisi Wasaidizi wa mikoa.

#### 3.2.8.3 Taasisi za Benki

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia taasisi za benki ili kukuza mitaji, amana na ukwasi na hivyo kuchochea kasi ya utoaji wa mikopo ya uwekezaji na biashara ya muda mfupi, wa kati na mrefu kama ifuatavyo:

##### 3.2.8.3.1 Benki za Maendeleo

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** benki za maendeleo zinajumuisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB na Benki ya Maendeleo TIB. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, TADB imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 47.17 kwa miradi 106 iliyowanufaisha wakulima 236,605 katika mikoa

20, ikiwemo Zanzibar. Hivyo, jumla ya mikopo iliyotolewa tangu TADB ilipoanzishwa imefikia shilingi bilioni 250.0 na wanufaika 1,794,452. Mikopo iliyotolewa imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazao ya mahindi, mpunga, mtama, alizeti, mbogamboga na matunda, kahawa, korosho, pamba, karafuu, asali pamoja na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ng'ombe wa nyama, kuku na samaki.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mikopo na huduma za moja kwa moja zilizotolewa, TADB imewezesha upatikanaji wa mikopo ya shilingi bilioni 24.5 kutoka katika benki na taasisi za fedha kupitia udhamini wa Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) na kufanya jumla ya mikopo iliyodhaminiwa kufika shilingi bilioni 75.03 tangu mfuko wa SCGS ulipoanzishwa rasmi mwaka 2018. Mikopo hiyo imenufaisha wakulima 10,894, AMCOS 153 na viwanda vidogo (SMEs) 32 vinavyonunua na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wadogo.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa benki ya Maendeleo TIB, hadi Machi 2021, benki imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 640.17, sawa na ongezeko la asilimia 1.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 628.11 iliyotolewa katika kipindi kilichoishia Machi 2020. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: madini ya dhahabu na ujenzi(shilingi bilioni 170.07), kilimo (shilingi bilioni 161.63), utalii (shilingi bilioni 70.55), uzalishaji (shilingi bilioni 63.94), Majengo (shilingi bilioni 50.54), biashara (shilingi bilioni 24.72), umeme (shilingi bilioni 21.56), Hoteli (shilingi bilioni 17.11), elimu (shilingi bilioni 15.10), gesi (shiling bilioni 13.22), Taasisi za fedha (shilingi bilioni 9.46), usafirishaji na mawasiliano (shilingi bilion 6.85), mikopo binafsi (shilingi bilioni 5.52), ujenzi (shilingi bilion 3.88), huduma nyingine (shilingi bilioni 2.55), maji (shilingi bilioni 2.37), ukodishaji mali (shilingi bilioni 0.8) na uvuvi (shilingi bilioni 0.29). Jumla ya

miradi iliyonufaika na mikopo hiyo ni 102.

#### 3.2.8.3.2 Benki ya Biashara ya TPB

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Benki ya TPB ilipanga kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 633.7 na kukuza amana kufikia shilingi bilioni 818. Hadi Aprili 2021, TPB benki imekusanya amana za jumla ya shilingi bilioni 888 sawa na ufanisi wa asilimia 108.5 na kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 618, ikiwa ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.5. Maeneo yaliyonufaika na dhamana na mikopo hiyo ni pamoja na: Wajasiliamali wakubwa na wakati, wastaafu, waajiriwa na vikundi vya akina mama na vijana.

#### 3.2.8.3.3 Taasisi za Bima

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania – *TIRA* inasimamia sekta ya bima nchini. Hadi Aprili 2021, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imetekeleza yafuatayo: kukagua watoa huduma za bima, zikiwemo kampuni 18 na matawi ya kampuni za bima 22, madalali watatu (3), mawakala 132 na vyombo vya moto 1,685; kutolea ufumbuzi malalamiko 26 ya bima yaliyopokelewa; kuandikisha na kutoa leseni 812 ambapo kati ya hizo, jumla ya kampuni zilizoandikishwa ni 23, Madalali 59, wakala 663, na wakadiriaji wa bima 48; na kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Madai ya Bima.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Bima la Taifa limefanikiwa kufunga mfumo wa *Enterprise Resource Management System (ERMS)* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuimarisha usimamizi wa taarifa za kihasibu na kuanza kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Bima katika matawi yake yote. Mifumo hiyo kwa pamoja

itaongeza ufanisi na uwazi katika utunzaji wa taarifa za wateja, ulipaji wa madai, utunzaji sahihi wa taarifa za kihasibu pamoja na kuwezesha wateja kukata bima na kuwasilisha madai yao kupitia simu za mkononi.

#### 3.2.8.3.4 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia mifuko miwili ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ni Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - *UTT AMIS* na Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha *(Self Microfinace Fund).* Lengo la kuanzishwa kwa mifuko hiyo ni kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi wenye kipato cha chini ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali, kujiongezea kipato na hatimaye kuondokana na umaskini wa kipato.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, UTT AMIS imefanikiwa kuongeza rasilimali za mifuko kutoka shilingi bilioni 362.83 hadi shilingi bilioni 542.9, sawa na ongezeko la asilimia 49.6, ikilinganishwa na lengo la asilimia 15; kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji kutoka wawekezaji 153,070 hadi 167,781, sawa na asilimia 9.6, ikilinganishwa na lengo la asilimia 5. Mafanikio hayo yametokana na utekelezaji mzuri wa mkakati wa elimu kwa umma kuhusu faida na umuhimu wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF umetoa mikopo ya shilingi bilioni 29.3, sawa na asilimia 89 ya lengo la kutoa shilingi bilioni 32 kwa kipindi cha miezi tisa. Kiasi hicho cha mikopo kimetolewa kwa wajasiriamali wadogo 11,387, ambapo wanawake ni 6,148, sawa na asilimia 54 na wanaume 5,238, sawa na asilimia 46. Mikopo iliyotolewa imeelekezwa katika sekta ya Kilimo (shilingi bilioni 2.9) na Viwanda Vidogo na

Biashara (shilingi bilioni 26.4). Kiwango cha urejeshaji mikopo kilifikia asilimia 95 sawa na matarajio ya kiwango kisichopungua asilimia 95. Hali hiyo imechangiwa na wateja wengi kuelekeza fedha katika shughuli za uzalishaji ambapo walirejesha mikopo kwa wakati. Aidha, Mfuko kwa kushirikiana na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umetoa mafunzo ya kujenga uelewa wa masuala ya fedha kwa wajasiriamali wadogo wapatao 310. Mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya fedha na huduma zitolewazo na Mfuko wa SELF.

### 3.2.6 Taasisi za Mafunzo, Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inasimamia Taasisi za mafunzo, elimu ya juu na Bodi za kitaaluma ambazo ni: Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP; Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC; Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA; Chuo cha Uhasibu Arusha – IAA; Chuo cha Kodi - ITA; Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA. Taasisi hizo zimepewa jukumu la kutoa mafunzo, kuendeleza wataalamu na wanataaluma, kufanya tafiti, na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya mipango, kodi, usimamizi wa fedha, takwimu na ununuzi na ugavi.

#### 3.2.6.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21; taasisi za mafunzo ya elimu ya juu zimedahili jumla ya wanafunzi 59,535, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 15,024, ikilinganishwa na wanafunzi 44,511 waliodahiliwa mwaka 2019/20. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi waliodahiliwa kwa ngazi ya cheti ni 13,336, stashahada 13,955, shahada 21,755 na uzamili 10,489.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, takwimu zinaonesha kuwa, kuna ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kozi za mipango, uhasibu, takwimu na ununuzi na ugavi, ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la miundombinu, idadi ya wakufunzi na nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni na majengo ya utawala kama ifuatavyo: Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kimekamilisha ujenzi na kuanza kutumia majengo ya utawala, madarasa, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Kanda ya Ziwa – Simiyu; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kimekamilisha ujenzi wa kumbi za mihadhara, madarasa na ofisi katika kampasi ya Kanda ya Ziwa – Mwanza; Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kinaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wa *Post Graduate* na mabweni manne (4) ya wanafunzi katika kampasi ya Arusha. Aidha, Chuo cha Uhasibu Arusha kimeanza ujenzi wa madarasa na hosteli mbili (2) katika kampasi ya Babati.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kimefanya maboresho ya madarasa kwa kufunga viti vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 100 badala ya wanafunzi 40; kusambaza huduma ya intaneti (wireless) ili kuwezesha walimu kutoa mafunzo au kufundisha kwa njia ya mtandao; na kukamilisha maandalizi ya mitaala mipya kwa ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada ili kuwezesha udahili wa wanafunzi wengi katika fani za takwimu rasmi, uchumi na TEHAMA.

### 3.2.6.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB imetekeleza

yafuatayo: kudahili watahiniwa 1,696 katika ngazi anuai za mitihani; kusajili wataalamu 1,163 wa ununuzi na ugavi katika ngazi mbalimbali; na kuendelea kusimamia mienendo na maadili ya wataalamu kwa kuendesha vikao vya maadili na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wataalamu wanaokiuka miiko ya taaluma ya ugavi na ununuzi.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA, hadi Aprili 2021, bodi ilifanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha katika taasisi 51; kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani kwa watahiniwa 11,247. Kati ya hao, watahiniwa 42 walifaulu mitihani ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu na 666 Shahada ya Juu ya Uhasibu. Aidha, NBAA ilitoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini kwa wahitimu 165; kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi kwa taasisi za umma na binafsi tisa (9) Tanzania Bara; kufanya ukaguzi wa kampuni 45 za uandaaji na ukaguzi wa hesabu; na kusajili watunza vitabu wawili (2). Vile vile, NBAA imeendesha mafunzo ya uzoefu kazini kwa wahasibu wahitimu 666, wahasibu ngazi ya CPA 67, wakaguzi hesabu katika ngazi ya CPA-PP 26 na kampuni mbili (2) za ukaguzi wa hesabu na uhasibu.

### 3.2.7 Usimamizi wa Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na jukumu la kusimamia utatuzi wa migogoro ya kodi na ununuzi wa umma kupitia Bodi ya Rufani za Kodi- TRAB, Baraza la Rufani za Kodi-TRAT na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Ununuzi wa Umma – PPAA ili kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria. Hadi Aprili 2021, Bodi ya Rufani za Kodi imesajili jumla ya kesi 653 zenye kiasi cha kodi inayobishaniwa ya shilingi 2,768,010,559.36 na imesikiliza na kutolea maamuzi

ya jumla ya kesi 542 zenye kiasi cha kodi inayobishaniwa ya shilingi 4,593,505,093,966.14. Kesi zilizoisha mwaka 2013 - 2019 zimefanyiwa uhariri wa mwanzo ili kuwasilishwa kwa Mhariri na hatimaye kuandaa ripoti za kesi za kodi zitakazotumika kama rejea.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2021, Baraza la Rufani za Kodi limefanikiwa kusikiliza na kutolea maamuzi kesi 143 kati ya 147 zenye kodi inayobishaniwa ya shilingi 1,373,228,849,228.58 na Dola za Kimarekani 1,450,920 na kesi 116 zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Aidha, Baraza linaandaa Mfumo wa Takwimu za Mashauri kwa ajili ya kuhifadhi na kutunza kumbukumbu za mashauri ya rufaa za kodi. Vile vile, Wizara imeziwezesha taasisi za rufani za kodi (TRAB na TRAT) kufanya ukarabati wa jengo la ofisi unaotarajiwa kukamilika Juni 2021.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imepokea jumla ya mashauri 28 ambayo ni sawa na asilimia 93 ya rufaa zilizokadiriwa kwa mwaka. Mashauri 27 kati ya - 28 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, mashauri yote yameamuliwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.

### 3.2.8 Tume ya Pamoja ya Fedha

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Pamoja ya Fedha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri wa masuala ya fedha yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi Aprili 2021, Stadi ya Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta za Uchumi na Mapato ya Muungano imefanyika na mapendekezo kuwasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika kwa maamuzi. Kazi nyingine zilizofanyika ni uchambuzi wa takwimu za Mapato na Matumizi ya Muungano na kutoa

mafunzo kuhusu mahusiano ya masuala ya fedha kwa Wajumbe wanne (4) wa Sekretarieti ya Tume.

### 3.2.9 Sekta ya Michezo ya kubahatisha

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha – *GBT* imeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa michezo ya kubahatisha ili kudhibiti mwenendo wa michezo ya kubahatisha, ikiwa ni pamoja na kuongeza mchango wa tasnia hiyo katika mapato ya Serikali na uchumi kwa ujumla.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imefanikiwa kufanya yafuatayo: kuunganisha mifumo ya udhibiti wa michezo ya kubahatisha ya *Gaming Licensing, Inspection and Compliance - GLICA* na *Gaming Regulatory Monitoring System- GREMS* na mifumo ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Mfumo wa Usajili wa Kampuni unaosimamiwa na *BRELA;* kutoa leseni 3,243, kati ya hizo, leseni mpya ni 1,019 na leseni 2,224 zilihuishwa; na kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha. Aidha, Bodi imekamilisha utengenezaji wa moduli zote za mfumo wa udhibiti wa *GREMS* utakaowezesha kufunga Mfumo wa Kudhibiti Mashine za Kuendesha Michezo ya Kubahatisha - SIGMa ambao upo katika hatua za mwisho za majaribio. Kipindi cha majaribio kinatarajiwa kukamilika Juni 2021 na hivyo kutoa fursa kwa zoezi la kufunga SIGMA katika mashine zote za kuendesha michezo ya kubahatisha kuanza Julai 2021.

### 3.2.10 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu ilipanga

kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Sheria ya Kampuni, hususan kipengele cha taarifa za umiliki wa kampuni. Hadi Aprili 2021, Kitengo kimewasilisha mapendekezo ya maeneo mahususi ya marekebisho ya sheria kwenye Kamati ya Kitaifa ya Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi. Aidha, Kitengo kimeboresha mifumo ya upokeaji wa taarifa za miamala shuku, fedha taslimu na usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huo umewezesha Kitengo kupokea na kuchambua: tarifa 738 za miamala shuku; tarifa 1,526 za usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo mipakani; taarifa 2,374 za miamala ya fedha taslim na taarifa 2,374 za utumaji na upokeaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki. Uchambuzi huo umewezesha Kitengo kuwasilisha taarifa fiche 79 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa hatua za uchunguzi.

### 3.2.11 Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kudhibiti Ununuzi wa Umma, ambapo jukumu hilo limekasimiwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma – PPRA na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini- GPSA.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi ya Umma- PPRA ilipanga kuendelea kusimamia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao- TANePS na kufanya ukaguzi wa Ununuzi wa Umma kwa taasisi nunuzi ili kutathmini kiwango cha ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410. Hadi Aprili 2021, Mamlaka imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo kwa watumishi 942 na kusajili wazabuni 17,149 kwenye mfumo wa TANePS. Aidha, PPRA imekamilisha ukaguzi wa Ununuzi uliofanywa na taasisi nunuzi 105 kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo matokeo yanaonesha kuwa kiwango cha ukidhi wa sheria

kimeongezeka kutoka asilimia 76 mwaka 2018/19 hadi asilimia 78.8 mwaka 2019/20.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – GPSA ilipanga kutekeleza yafuatayo: Kufanya ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja ili kupunguza gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji na kujenga matanki mawili (2) ya kuhifadhi mafuta mkoani Mtwara (1) na Mbeya (1). Hadi Aprili 2021, wakala umefanya ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali 794 na pikipiki 37 kwa shilingi. 98,485,529,619.38 kwa niaba ya taasisi nunuzi 199. Kwa utaratibu huo, Serikali imeokoa shilingi 4,925,539,988.34. Kati ya hizo shilingi 1,288,525,000 kutokana na unafuu wa michakato ya ununuzi wa pamoja na shilingi 3,637,014,988.34 ni punguzo la bei kwa ununuzi wa pamoja. Aidha, wakala umesimika tanki mkoani Mtwara lenye ujazo wa lita 30,000 na usimikaji wa tanki lenye lita 40,000 katika mkoa wa Mbeya unaendelea.

### 3.2.12 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**62.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2020/21 Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kufanya Sensa za Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa mwaka 2019/20; kufanya utafiti wenye lengo la kubaini Watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2020/21; kutenga maeneo ya kuhesabia watu nchini, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi linalotarajiwa kufanyia mwezi Agosti 2022; na kutoa takwimu za Msingi katika maeneo ya uchumi.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2021, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanikiwa kutoa matokeo ya awali kuhusu Sensa ya majaribio iliyofanyika katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2019/20. Aidha, Ofisi imeendelea kutenga

maeneo ya kuhesabia watu katika wilaya ya Chamwino, Bahi, Kondoa, Kongwa, Chemba na Singida Mjini; kutoa takwimu za Mfumuko wa Bei kwa mwezi Julai hadi Aprili 2020; kutoa fahirisi ya uagizaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kuanzia mwezi Januari 2020 hadi Septemba 2020 na kutoa takwimu za Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani kwa mwezi Januari 2020 hadi Septemba 2020.

#### 3.2.6 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2021 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi kwa mafungu ya Wizara na Idara za Serikali 66; Wakala 34; Taasisi 53; Vyama vya siasa 19; Bodi za mabonde ya maji 15; Hospitali 32 za rufaa za Mikoa; Sekretarieti za Mikoa 26; Mamlaka za Serikali za Mitaa 185; Mashirika ya Umma 165; na Mifuko Maalumu 16. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa jumla ya miradi ya maendeleo 303, ambapo ripoti 290 za fedha na 13 za kiufundi zilitolewa katika miradi husika. Vile vile, Ofisi imefanya kaguzi maalumu 3 na ripoti zake zimeandaliwa.

## 3.3 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo

### 3.3.1 Changamoto

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na majukumu yaliyotekelezwa Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ugumu wa kutoa viwango stahiki vya fidia (*fair compensation)* kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali kutokana na kukosekana kwa sheria au mwongozo wa viwango vya fidia zinazohusisha mali za Serikali;

(ii) Baadhi ya maeneo kutofikiwa na huduma za mtandao ambazo ni kiungo kikuu cha matumizi ya mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi;

(iii) Kuongezeka kwa vihatarishi vya kudukuliwa kwa mifumo ya fedha na watu wenye nia ovu; na

(iv) Mgongano wa maslahi kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu katika kusimamia mapato, matumizi na mali za serikali.

### 3.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na:

i. Kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria au Mwongozo wa Ulipaji Fidia kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali;
ii. Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ambayo itabainisha mipaka ya usimamizi wa fedha kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mamlaka za Mitaa;
iii. Mamlaka husika kuongeza wigo wa mtandao wa mawasiliano hadi kwenye maeneo ya vijijini ambayo hayajafikiwa;
iv. Kuimarisha vituo vya usalama wa mifumo (*Disaster Recovery Sites*) pamoja na kuandaa na kusimamia miongozo ya usalama wa mifumo; na
v. Kutoa elimu na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali katika ngazi zote za utumishi wa umma.

## 4.0 VIPAUMBELE NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/22

### 4.1 Vipaumbele vya Mafungu (07,10,13,21,22,23,45 &50)

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango, ikiwemo Ofisi ya Taifa ya

Ukaguzi inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Muda wa Kati wa Mapato na Matumizi (MTEF). Katika vipaumbele vya matumizi ya kawaida, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo:

i. Kufanya mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26) na kuanza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;
ii. Kufanya tafiti za kiuchumi na modeli za fedha ili kubaini fursa fiche za uwekezaji na vyanzo vipya vya mapato, ikiwa ni pamoja na mapato ya kugharamia shughuli za Muungano;
iii. Kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali ili kubaini maeneo yenye upungufu au changamoto na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua;
iv. Kufanya tathmini ya Uhimilivu wa deni la Serikali (DSA);
v. Kuratibu mipango na mikakati ya upatikanaji wa misaada, mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali;
vi. Kutunga Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Benki na Mkakati wake;
vii. Kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2022/23 - 2026/27);
viii. Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi, Tathmini na Ufuatiliaji wa Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma;
ix. Kufanya ufuatiliaji, tathmini, ukaguzi, udhibiti na uhakiki wa mapato, matumizi, miradi ya maendeleo, mali za umma; na miamala ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;
x. Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya PPP;
xi. Kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;
xii. Kufanya sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2022; na
xiii. Kutunga Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na Mkakati wa utekelezaji wake.

**68.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo:

i. Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mikataba, Ufuatiliaji na Tathmini, Usimamizi wa Vihatarishi vya Deni la Serikali pamoja na Vihatarishi vya Ununuzi wa Umma;
ii. Kuhuisha na kufungamanisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha na mali za umma ili kudhibiti upotevu wa mapato na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kurahisisha upatikanaji na usuluhishi wa taarifa za fedha;
iii. Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Bahari (*National Strategy for Blue Economy*);
iv. Kuwajengea uwezo watumishi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali;
v. Kuimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali; na
vi. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli pamoja na jengo la Ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Geita.

## 4.2 Vipaumbele vya Taasisi

**69.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/22, Taasisi zilizo chini ya Wizara zinatarajia kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza tija katika uchumi na utoaji huduma kama ifuatavyo:

### 4.2.1.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu zinatarajia kufanya yafuatayo: Kudahili jumla ya wanafunzi 65,322, wakiwemo ngazi ya cheti 14,545, stashahada 17,735, shahada 31,602 na uzamili 1,440; kuendeleza shughuli za utafiti pamoja na mafunzo kwa

watumishi; na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM kinatarajia kuendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa Kampasi ya Simiyu kwa kujenga nyumba za watumishi nne (4) mabweni mawili (2) na uzio; kuanza ujenzi wa mabweni pamoja na majengo ya Shule ya Biashara Njedengwa, Jijini Dodoma; kukamilisha ununuzi wa ardhi mkoani Mwanza kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mwanza; kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Kampasi ya Dar es Salaam; na kuendelea na Ujenzi wa Kampasi ya Geita.

**72.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/22, Chuo cha Uhasibu Arusha- IAA kinatarajia kutekeleza yafuatayo: kukamilisha Ujenzi wa jengo la Uzamili, mabweni manne (4), vyumba vya madarasa vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,800 katika kampasi kuu Arusha na Ujenzi wa madarasa na jengo la utawala kampasi ya Babati. Aidha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP kinatarajia kumalizia ujenzi wa jengo la taaluma, bweni la wasichana, mgahawa na maktaba katika kampasi ya Mwanza; na kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma, bweni la wasichana awamu ya II na kujenga jengo la taaluma katika kampasi ya Dodoma.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Taaluma Kampasi ya Dar es Salaam na maktaba Kampasi ya Singida; kuanza ujenzi wa hosteli, madarasa, nyumba za watumishi na maktaba katika Kampasi ya Mjimwema - Mtwara; na kuanza ujenzi wa Jengo la Taaluma Kampasi ya Mwanza. Aidha, Wizara imejipanga kuziwezesha Taasisi zote za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara kusimika mifumo ya TEHAMA ya kufundishia na

kujifunza katika mwaka 2021/22.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Chuo cha Kodi - ITA kinatarajia kuendelea na upanuzi wa jengo la utawala, ujenzi wa hosteli ya wafanyakazi wanaohudhuria mafunzo ya muda mfupi yanayotolewa na chuo, na kukamilisha *Master plan* ya Kampasi ya Misugusugu - Kibaha.

#### 4.2.1.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi katika ngazi anuai za usajili, kuendesha mitihani ya kitaaluma mara mbili kwa mwaka kwa watahiniwa 4,000 na kuendesha mafunzo endelevu yaani CPD 24 kwa wataalamu 3,000. Aidha, Bodi ya NBAA inatarajia kuendelea kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha nchini, kuendeleza taaluma ya uhasibu na kutoa mitihani, kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi, kusimamia ubora wa wakaguzi wa hesabu, kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu zinazohusu taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu.

#### 4.2.1.3 Taasisi za Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma

**76.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2021/22, taasisi za rufani za kodi na ununuzi wa umma ambazo ni *TRAB, TRAT* na *PPAA* zitaendelea kupokea, kusajili, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufani za kodi na ununuzi. Aidha, *PPAA* imepanga kuandaa mkakati wa vyanzo vingine vya mapato (*Revenue Enhancement Strategy*) ili kuongeza wigo wa Mapato kwa Mamlaka.

### 4.2.1.4 Bodi ya Michezo ya kubahatisha

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/22 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha itaendelea kutoa leseni 11,367 kwa waendesha michezo ya kubahatisha ambapo katika hizo 7,408 ni leseni mpya na 3,959 ni leseni zitakazo huishwa, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 76 na kutoa elimu ili ushiriki katika michezo ya kubahatisha uwe ni wa kiasi na wa kujitambua.

### 4.2.1.5 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22, Mamlaka ya Mosoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Bidhaa zitaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi, udhibiti na uendeshaji wa masoko hayo; kuandaa miongozo ya mazao yatakayouzwa sokoni kwa kushirikiana na wadau husika; kuongeza idadi ya mazao yatakayouzwa kupitia Soko la Bidhaa ambapo mazao hayo ni: Chai, Mkonge, Kakao, Pamba, Kahawa, na vitunguu. Aidha, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana inatarajia kufanya maboresho au kutunga sheria mpya ya udhibiti wa masoko ya mitaji na dhamana hapa nchini.

### 4.2.1.6 Taasisi za Benki

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatarajia kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 203.5 kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wanaojishughulisha na usambazaji wa pembejeo, zana, uzalishaji, uchakataji, ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, Benki ya MaendeleoTIB imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 54.585 katika sekta ya Viwanda, Maji, Nishati, Utalii, Kilimo, Elimu na Miundombinu ya Serikali za Mitaa.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya benki ya TPB katika mwaka 2021/22 ni: Kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 647; kuboresha uwezo wa benki wa kuzalisha mapato yake ili kufikia shilingi bilioni 181.4; faida kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 18.4; amana za benki kufikia shilingi bilioni 707; mali za benki kufikia shilingi bilioni 1,014; na thamani ya hisa kukua na kufikia shilingi bilioni 118 Desemba 2021.

#### 4.2.1.7 Taasisi za Bima

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania- *TIRA* katika mwaka 2021/22 ni: kuboresha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa mapato (*TIRA RBS na TIIP*); kufanya ukaguzi wa kampuni 30 za bima; kufanya upekuzi wa ndani wa mapato kwa kampuni 10 zinazotoa huduma za bima; Kutoa elimu ya masuala ya bima kwa umma ili kuongeza uelewa kutoka asilimia 36 hadi asilimia 40; kuchochea matumizi ya huduma za bima kwa umma ili kuwafikia Watanzania milioni 1.5 na kuhamasisha kampuni 30 za bima kuandaa bidhaa zisizopungua mbili (2) zinazokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, vipaumbele vya Shirika la Taifa la Bima ni: kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa huduma za bima; kuboresha uwezo wa uandikishaji wa wateja wa bima; na kulipa bima zilizoiva pamoja na madai kwa wakati; na kuhamasisha na kufuatilia uandikishaji wa bima kwa taasisi za umma.

#### 4.2.1.8 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Mfuko wa Uwekezaji wa UTT AMIS unatarajia: kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; na kuzindua rasmi huduma za

usimamizi wa mitaji binafsi (*Wealth Management Services*). Aidha, Mfuko wa *SELF* unatarajia: kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 32.00, kuwafikia wajasiriamali wadogo wapatao 28,255 kwa huduma za kifedha na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wapatao 265.

#### 4.2.1.9 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Ofisi ya Taifa inatarajia kukamilisha maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 2022 kwa kuendelea kutenga maeneo ya kuhesabia watu; kufanya utafiti wa Afya ya Uzazi, Mtoto na Malaria; Kufanya maandalizi ya Awamu ya Pili ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Takwimu Nchini; na kuendelea kutoa takwimu za msingi za uchumi.

#### *4.2.1.10* Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma – *PPRA* inatarajia: Kutoa mafunzo kwa watumishi 1,200 kutoka kwa Taasisi Nunuzi 300 na wazabuni 1,200 ambao wamejisajili kwenye mfumo wa Ununuzi (*TANePS*); kufanya ukaguzi wa Ununuzi kwa taasisi 180; kufuatilia uzingatiaji wa mikataba ya Ununuzi kwa taasisi nunuzi 120 na kufanya tathmini ya Uwezo wa Ununuzi wa taasisi nunuzi tano (5) (*Procurement Capability Assessment).*

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – *GPSA* itaendelea na: Ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja; kuandaa mikataba maalumu ya ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa niaba ya taasisi za Serikali; kugomboa na kuondosha mizigo ya serikali bandarini, viwanja vya ndege na

mipakani; na kujenga matanki matatu (3) Kurasini- Dar es Salaam kwa ajili ya uagizaji wa mafuta moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

### 4.3 Makadirio ya Mapato

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 920,377,606,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na mauzo ya nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa na Mafungu ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na.2: Maduhuli Yanayokadiriwa Kukusanywa na Mafungu ya Wizara kwa mwaka 2021/22**

| Fungu | Jina la Fungu | Kiasi |
|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 860,077,606,000 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 60,000,000,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 300,000,000 |
| **JUMLA** | | **920,377,606,000** |

### 4.4 Makadirio ya Matumizi

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2021/22, ni mwaka wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2017/18 – 2021/22). Hivyo, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango huo na kubaini kuwa, baadhi ya shabaha zinahitaji nyongeza ya rasilimali fedha ili kufikia malengo tarajiwa. Kwa muktadha huo, Wizara imechukua hatua ya kuimarisha bajeti ya baadhi ya kasma katika mwaka 2021/22 ili kuchochea kasi ya utekelezaji wa shabaha za Mpango Mkakati na hivyo kufikia malengo ifikapo Juni 2022. Kasma zilizoimarishwa kibajeti ni pamoja na:

ukaguzi wa ndani; mifumo ya usimamizi na udhibiti wa fedha na mali za Serikali; tafiti za kiuchumi na modeli za fedha; ufuatiliaji na tathmini; usimamizi wa deni la Serikali; uhakiki na ulipaji wa madeni na madai ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma; na kuziwezesha taasisi chini ya Wizara kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vya mwaka 2021/22 kwa ufanisi, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **shilingi 12,961,271,473,000** kwa Mafungu yote saba (7). Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,935,643,022,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,025,628,451,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/22, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 80,099,935,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 68,185,033,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 11,914,902,000** matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi 13,346,294,000** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 54,838,739,000** matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi 9,200,000,000** fedha za ndani na **shilingi 2,714,902,000** fedha za nje. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na.3.**

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22**

| FUNGU NA. | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA-MATUMIZI YA KAWAIDA | NDANI | NJE | JUMLA-MAENDELEO | |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 3,859,834,000 | 57,229,786,000 | 61,089,620,000 | 1,000,000,000 | 1,300,000,000 | 2,300,000,000 | 63,389,620,000 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 716,795,000 | 2,048,142,000 | 2,764,937,000 | - | - | - | 2,764,937,000 |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu | - | 2,915,586,000 | 2,915,586,000 | | 400,000,000 | 400,000,000 | 3,315,586,000 |
| 21 | HAZINA | 216,420,214,000 | 855,911,377,000 | 1,072,331,591,000 | 975,013,499,000 | 24,034,036,000 | 999,047,535,000 | 2,071,379,126,000 |
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | 9,275,296,000 | 10,664,243,143,000 | 10,673,518,439,000 | - | - | - | 10,673,518,439,000 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 5,967,732,000 | 38,551,734,000 | 44,519,466,000 | 2,000,000,000 | 1,669,650,000 | 3,669,650,000 | 48,189,116,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 7,799,526,000 | 70,703,857,000 | 78,503,383,000 | 14,208,880,000 | 6,002,386,000 | 20,211,266,000 | 98,714,649,000 |
| **JUMLA - MAFUNGU YOTE** | | **244,039,397,000** | **11,691,603,625,000** | **11,935,643,022,000** | **992,222,379,000** | **33,406,072,000** | **1,025,628,451,000** | **12,961,271,473,000** |
| | | | | | | | | |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 13,346,294,000 | 54,838,739,000 | 68,185,033,000 | 9,200,000,000 | 2,714,902,000 | 11,914,902,000 | 80,099,935,000 |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## 5.0 HITIMISHO

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi. Hamad Yussuf Masauni, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni- Zanzibar na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vile vile, nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Bw. Emmanuel M. Tutuba na Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bw. Adolf H. Ndunguru na Dkt. Khatib M. Kazungu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vile vile, nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na watumishi wote wa taasisi hizo kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Fedha na Mipango.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.mof.go.tz.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho Na.1: Fedha zilizotumika kwa Mishahara hadi Aprili 2021**

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2020/21 | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi Aprili, 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Mishahara ya Idara/Vitengo | 7,582,493,000.00 | 5,632,649,921.91 | 74 |
| | | Ruzuku ya Mishahara Taasisi | 31,655,505,000.00 | 22,204,237,086.00 | 70 |
| 21 | HAZINA | Mishahara ya Idara/Vitengo | 5,726,241,000.00 | 4,315,863,605.68 | 75 |
| | | Ruzuku ya Mishahara Taasisi | 199,795,582,000.00 | 159,084,414,343.98 | 80 |
| | | Marekebisho ya Mishahara ya Watumishi wa Umma | 245,380,127,000.00 | 107,896,701,453.34 | 44 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | | 3,375,080,000.00 | 2,623,537,188.47 | 78 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 802,823,000.00 | 591,843,547.00 | 74 |
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 9,989,416,000.00 | 6,057,870,762.01 | 61 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 5,738,683,000.00 | 4,352,993,720.00 | 76 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | | 14,883,256,000.00 | 10,766,951,058.00 | 72 |
| **Jumla -Mishahara** | | | **524,929,206,000.00** | **323,527,062,686.39** | **62** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

**Kiambatisho Na. 2: Fedha zilizotumika kwa Matumizi Mengineyo hadi Aprili 2021**

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2020/21 | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi Aprili, 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 10,477,797,406,000.00 | 7,426,931,060,855.00 | 71 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | Uendeshaji wa Ofisi | 10,229,786,000.00 | 8,401,716,304.96 | 82 |
| | | Matumizi Maalum | 12,000,000,000.00 | 5,401,763,583.88 | 45 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 2,048,142,000.00 | 1,706,785,000.00 | 83 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | | 2,915,586,000.00 | 1,720,245,196.68 | 59 |
| 21 | HAZINA | Idara/Vitengo | 36,902,902,000.00 | 26,460,449,777.59 | 72 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 141,152,667,000.00 | 117,627,222,499.90 | 83 |
| | | Matumizi Maalum | 459,220,293,000.00 | 365,895,468,564.81 | 80 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Idara/Vitengo | 23,313,168,000.00 | 19,052,057,202.14 | 82 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 4,479,346,000.00 | 4,079,854,687.47 | 91 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 58,036,734,000.00 | 40,996,443,295.00 | 71 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | | 53,993,739,000.00 | 41,858,487,424.00 | 78 |
| **Jumla - Matumizi Mengineyo** | | | **11,282,089,769,000.00** | **8,060,131,554,391.43** | **71** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

## Kiambatisho Na.3:Fedha zilizotumika kwa Miradi ya Maendeleo hadi Aprili 2021

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2020/21 | | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi Aprili, 2021 | | Asilimia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,000,000,000.00 | 1,300,000,000.00 | 887,786,976.68 | 725,797,240.00 | 89 | 56 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 500,000,000.00 | - | - | - | - |
| 21 | HAZINA | 616,196,465,000.00 | 24,807,427,000.00 | 18,740,483,641.00 | 9,758,150,275.06 | 3.04 | 39 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 2,000,000,000.00 | 1,500,000,000.00 | - | 750,152,181.00 | - | 50 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 5,508,880,000.00 | 6,507,551,000.00 | 1,458,570,815.80 | 2,680,372,689.00 | 26 | 41 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 6,700,000,000.00 | 4,967,940,000.00 | 2,230,554,005.00 | 136,965,000.00 | 33 | 3 |
| **Jumla - Maendeleo** | | **631,405,345,000.00** | **39,582,918,000.00** | **23,317,395,438.48** | **14,051,437,385.06** | **4** | **35** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***